# VIGEZO NA TARATIBU ZA KUANZISHA/KUPANDISHA HADHI MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

## 1.0 UTANGULIZI

Mamlaka za Serikali za Mitaa huanzishwa kwa kuzingatia Ibara 145 na 146 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara hizi zinaelekeza kuanzishwa kwa vyombo vya Serikali za Mitaa katika eneo la Mikoa, Wilaya, Mji na Kijiji. Ili kutekeleza matakwa haya, **Sheria za Serikali za Mitaa zimeweka masharti, misingi na taratibu za kufuatwa katika kuanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa.**

## 2.0 MASHARTI NA TARATIBU

Utaratibu wa kuanzisha Mamlaka za Serikali za Mitaa ni mapendekezo au maombi ya kuanzisha Mamlaka hizo kupata ridhaa ya wananchi kupitia vikao vilivyowekwa Kisheria katika ngazi zifuatazo:

i. Vijiji,
ii. Kata (Kamati ya Maendeleo ya Kata - WDC);
iii. Halmashauri (Baraza la Madiwani),
iv. Wilaya (Kamati ya Ushauri ya Wilaya –DCC na
**v.** Mkoa (Kamati ya Ushauri ya Mkoa - RCC).

## 3.0 VIGEZO VYA KUZINGATIA KATIKA KUANZISHA MAENEO MAPYA YA UTAWALA NGAZI ZA CHINI ZA SERIKALI ZA MITAA

### 3.1 Vigezo vya kuanzisha Kitongoji

i. Kaya zisizopungua 50

**ii.** Kifungu cha 30 cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) inaelekeza kwamba eneo la Kijiji litagawanywa katika Vitongoji visivyozidi 5 (vitano)**.**

iii. Kitongoji ni eneo la utawala katika Mamlaka za Serikali za Mitaa linalotokana na kugawa eneo la Kijiji au eneo la Mamalaka ya Mji Mdogo katika maeneo ya utawala ili kuweza kumudu usimamizi wa utawala katika eneo la Halmashauri.

iv. Eneo la Kitongoji ni eneo la Jimbo la Uchaguzi la Mwenyekiti wa Kitongoji ambaye huwakilisha Kitongoji katika Halmashauri ya Kijiji. Uongozi katika eneo la Kitongoji upo chini ya Mwenyekiti wa Kitongaji.

v. kifungu cha 13(3) cha Sheria hiyo hiyo kinaelekeza kwamba eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo itagawanywa katika Vitongoji kama Mamlaka hiyo ya Mji Mdogo itakavyoamua.

vi. Masharti na utaratibu wa kugawa

## 3.2 Vigezo vya kuanzisha Kijiji

(i) Kuwepo kwa eneo la kutosha kwa ajili ya matumizi ya Wananchi kwa sasa na baadaye

(ii) Vitongoji visivyopungua vitano (5);

(iii) Idadi ya Kaya zisizopungua 250;

(iv) Idadi ya watu wasiozidi 10,000;

(v) Upatikanaji wa huduma za jamii kama vile maduka ya rejareja yasiyopungua matano (5), soko, shule ya msingi, zahanati na kituo kidogo cha polisi

## 3.3 Vigezo vya kuanzisha Mtaa

i. Mtaa ni eneo la Mamlaka za Miji (Halmashauri ya Mji, Manispaa, na Jiji) linalotokana na kugawanywa kwa eneo la Kata ya Mjini katika maeneo ya utawala ili kurahisisha usimamizi wa shughuli za Utawala, Huduma na Maendeleo. Kwa mujibu wa Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji)

Namba 8 ya mwaka 1982 eneo la Mtaa hugawanywa kwa kuzingatia idadi ya Kaya au sura ya nchi Kijiografia.

ii. Mtaa huwa na Mwenyekiti wa Mtaa ambaye ndiye Kiongozi na mwakilishi wa Mtaa katika Kamati ya Maendeleo ya Kata.

**iii.** Idadi ya Kaya ambazo zinapaswa kuwepo katika kila Mtaa ni zisizopungua **Kaya 50.**

### 3.4 Vigezo vya kuanzisha Kata

(i) Idadi ya Vijiji vilivyosajiliwa visivyopungua vitano (5);

(ii) Ukubwa wa eneo la usiopungua kilometa za mraba 500,

(iii) Idadi ya watu wasiopungua 10,000;

(iv) Uwezo wa Halmashauri kumudu gharama za ongezeko la maeneo ya Utawala,

## 4.0 VIGEZO VYA KUANZISHA HALMASHAURI ZA WILAYA:

i. Kuwepo na idadi ya Kaya zinazotakiwa kwa eneo kuwa Halmashauri ya Wilaya;

ii. Kuwepo kwa idadi ya watu wanaotakiwa kwa eneo kuweza kutambuliwa kuwa Halmashauri ya Wilaya;

iii. Kuwa na eneo la ardhi ya kutosha kuendeleza shughuli za kiuchumi, kijamii na kimaendeleo katika Halmashauri ya Wilaya kiwango;

iv. Kuwepo na mapato yanayotarajiwa kukusanywa kama kodi au tozo nyingine zenye kutosheleza utoaji wa huduma muhimu pamoja na uendeshaji wa shughuli za Serikali katika eneo zima la Halmashauri ya Wilaya;

v. Kuwepo kwa huduma za kijamii na kiuchumi, kama vile shule, vituo vya afya, zahanati, maji, barabara kwa kuzingatia viwango vilivyowekwa kitaifa kwa kila sekta husika.

## 5.0 VIGEZO VYA KUANZISHA HALMASHAURI ZA MIJI, MANISPAA NA JIJI:

### 5.1 Vigezo vya ujumla

i. Jiografia ambayo inafanya utoaji huduma kwa Wananchi kuwa mgumu kwa sababu ya milima, mito, misitu, mabonde au Visiwa.
ii. Kuwepo kwa miundombinu inayohitajika kwa eneo la utawala kuanzishwa,
iii. Kuwepo kwa mtandao wa barabara za uhakika kuunganisha Makao Makuu ya eneo la utawala lililoanzishwa na maeneo mengine yenye kuhitaji kuhudumiwa na Makao Makuu,
iv. Uwezo wa Serikali wa kuanzisha eneo jipya la utawala,
v. Utayari wa Wananchi kuchangia uanzishaji wa eneo la utawala.

Aidha, ili maeneo hayo yaweze kuanzishwa/ kupandishwa hadhi vimewekwa vigezo kwa mujibu wa Sheria ya Mipango Miji Na 8 ya mwaka 2007 (The Urban Planning Act No 8 of 2007) Kipengele cha Tano cha Jedwali la Tano (Item number 5 of the Fifth Schedule) kama ifuatavyo:-

### 5.2 Vigezo vya kuanzisha Mamlaka ya Mji Mdogo (Township Authority)

Mamlaka ya Mji Mdogo ni Mamlaka ya Serikali za Mitaa iliyopo kwenye Mamlaka za Wilaya. Mamlaka hizi zinaanzishwa pale ambapo palikuwa ni Kijiji ambacho kimeanza kuendelezwa na kuwa na mazingira ya kimji. Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa amepewa madaraka ya kutangaza Kijiji au Vijiji vilivyofikia sifa zilizowekwa kuwa Mamlaka za Miji Midogo.

### 5.3 Vigezo vinavyotakiwa kuzingatiwa:

i. Kuwe idadi ya watu wasiopungua elfu kumi (10,000);
ii. Kuwe na huduma za jamii zifuatazo: Shule ya Sekondari, Kituo cha Afya na Mahakama ya Mwanzo;

iii. Kuwe na Soko pamoja na Maduka ya rejareja yasiyopungua matano (5); na

iv. Eneo liwe ni Makao Makuu ya Kata au Tarafa.

### 5.4 Vigezo vya kuanzisha Halmashauri ya Mji (Town Council)

i. Kuwe na watu wasiopunga 30,000.

ii. Mji uwe na uwezo wa kujiendesha angalau kwa asilimia 50% ya bajeti yake.

iii. Mji uwe na kiwango cha juu cha utoaji huduma ya hospitali, kuwe na shule ya Sekondari, kuwe na angalau maduka ya rejareja yenye leseni yasiyopungua 50, Kituo cha Polisi na pawe na Makao makuu ya Tarafa.

### 5.5 Vigezo vya kuanzisha Halmashauri ya Manispaa

i. Kuwe na watu wasiopungua laki moja (100,000)
ii. Kuwe na watu wasiopungua laki moja (100,000)
iii. Asilimia 30% ya wakazi wake wawe katika ajira isiyohusiana na kilimo ***(Non agricultural Sector)***
iv. Kuwe na walau kiwanda kikubwa kimoja *(Manufacturing industry)*
v. Kuwe na viwanda kadhaa vya ***"Processing***
vi. Asilimia Sabini (70%) ya matumizi ya Manispaa yatokane na vyanzo vya mapato ya Halmashauri ***(Own Sources).***
vii. Kuwepo na huduma za jamii zifuatazo:-
- Kituo cha Elimu ya Watu Wazima;
- Hospitali ya Rufaa;
- Chuo Kikuu;
- Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa;.na kiwe ni Kituo cha Taasisi za Kimataifa ***(Mult National organization.)***

### 5.6 Vigezo vya kuanzisha Halmashauri ya Jiji

i. Kuwe idadi ya watu wasiopungua laki tano (500,000);

ii. Kuwa na uwezo wa kujitegemea kwa asilimia tisini na tano (95%) kwa mapato yake ya ndani; na

iii. Kuwepo sifa nyingine zaidi ya sifa za kawaida za Manispaa kama vile maeneo ya kihistoria, maeneo ya utalii; Makao Makuu ya Mkoa; kituo cha shughuli za Kimataifa na nyinginezo.